

# Uzalishaji wa maziwa bado tatizo nchini

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MSAJILI wa Bodi ya Maziwa Nchini, Dk. George Msalya, amesema Tanzania bado inakabiliwa na uzalishaji mdogo wa maziwa, huku kiasi cha Sh. bilioni 22 kikitumika kila mwaka kuagiza maziwa nje ya nchi.

Aliyasema hayo alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari katika maadhimisho ya wiki ya maziwa ambayo hufanyika Juni mosi ya kila mwaka, kwa mwaka huu kitaifa yatafanyika jijini Tanga.

Alisema Tanzania inazalisha lita bilioni 3.4, ikigawanywa kwa idadi ya Watanzania, kila mtu atakunywa wastani wa lita 50 tu kwa mwaka wakati anapaswa kunywa lita 200.

"Kwa mujibu wa wataalamu wa afya mtu anatakiwa kunywa maziwa lita 200 kwa mwaka, hivyo bado kuna uhitaji mkubwa wa uzalishaji zaidi wa maziwa ni kinywaji muhimu kwa afya ya binadamu," alisema.

Hata hivyo, alisema bado uelewa ni mdogo kwa watu badala ya kunywa maziwa wanakwenda baa kunywa pombe wakati maziwa ni muhimu kuliko pombe.

"Tangu kuanzishwa kwa bodi hii mwaka 2005 Tanzania imepiga hatua katika uzalishaji wa maziwa, ambapo hadi mwaka 2015 kila mtu alikuwa anakunywa lita 40 hadi 45,"alisema.

Alisema hadi kufikia mwaka 2021 kila mtu anakunywa maziwa lita 50 kwa mwaka, katika pato la Taifa maziwa yanachangia kwa asilimia 30 huku katika sekta ya mifugo ikichangia kwa asilimia saba.

Dk. Msalya aliwataka Watanzania kuwa na uzalendo wa kutumia bidhaa za ndani za maziwa ili kuwainua wafugaji, wasindikaji na wachakataji wa bidhaa hiyo kwa kuwa zipo bidhaa nzuri za maziwa zinazotengenezwa nchini.

Aidha, alisema katika maadhimisho hayo yatalenga katika kufanya utafiti kuhusu tasnia ya maziwa, kujifunza namna ya kufuga ng'ombe bora wa maziwa na kugawa maziwa kwenye makundi mbalimbali ikiwamo wagonjwa waliopo hospitalini.

Scanned with CamScanner

WATUHUMIWA wa kusafirisha dawa za kulevya, raia wa Iran, wakipelekwa katika Mahakama ya Mkoa Lindi, jana. (Picha na Sophia Nyalusi).

# Siri unywaji maziwa lita 200 yafichuliwa

**Na ASHURA ASSAD**

TANZANIA bado ina uzalishaji mdogo wa maziwa kwa sababu ina uwezo wa kuzalisha lita bilioni 3.4.

Maziwa hayo yakigawanywa kwa idadi ya Watanzania, kila mtu atakunywa wastani wa lita 50 tu kwa mwaka badala ya lita 200 zinazoshauriwa.

Hayo yalisemwa na Msajili wa Bodi ya Maziwa Nchini, Dk. George Msalya, alipozungumza na gazeti hili kuelekea Maadhimisho ya Wiki ya Maziwa inayoanza leo hadi Juni 4, mwaka huu.

Alisema serikali imekuwa ikitumia sh. bilioni 22 katika uagizaji maziwa kutoka nje ya nchi kisha kuingizwa nchini kupitia taasisi zake.

Dk. Msalya alisema suala la unywaji maziwa kwa Watanzania, linaonekana kukosa hamasa licha ya serikali kutumia juhudi kubwa kutoa hamasa.

"Bado uelewa ni mdogo. Mtu badala ya kunywa maziwa, anakwenda baa kunywa pombe, wakati maziwa ni muhimu kuliko hiyo pombe," alisema.

"Maziwa ni mlo kamili, unaweza usile ugali, maji na vyakula vinginevyo kwa sababu yana protini ya kutosha, hivyo Watanzania wanapaswa kunywa maziwa kwa ajili ya afya zao," alisema.

Alieleza kuwa, maziwa ni biashara nzuri kama yatauzwa na kuhifadhiwa vizuri, ndiyo maana kuna kampuni kama Asasi na Tanga Fresh ambayo yamekuwa yakifanya biashara hiyo ya uuzaji na ununuaji wa maziwa.

Kwa mujibu wa Msajili huyo, maziwa huchangia ukuaji wa uchumi, ni mlo muhimu kwa afya, lakini uzalishaji mdogo husababisha uingizaji wa maziwa kutoka nje ya nchi kama vile ya unga na mengineyo.

Aidha, alisema uhamasishaji wa unywaji maziwa, umechangia kuongezeka hata mifugo, lakini imehamasisha kuongezeka kwa ulaji na usindikaji.

"Tulikuwa chini ya lita 50, lakini kwa sasa tuko juu ya 50 ambapo kwa sasa sekta ya mifugo, inachangia pato la taifa kwa asilimia 7.

Alisema kuwa, tangu kuanzishwa kwa bodi hiyo mwaka 2005, Tanzania imepiga hatua katika uzalishaji wa maziwa, kwani mwaka 2015 kushuka chini, wastani kila mtu alikuwa anakunywa lita 40 hadi 45.

"Kufikia mwaka 2015 hadi 2021, kila mtu atakunywa maziwa lita 50 kwa mwaka, ambapo katika pato la taifa maziwa yanachangia asilimia 30."

**WANANCHI WAONGEA**

Juma John ambae ni dereva wa bodaboda kituo cha Lumumba, alisema elimu ni ndogo juu ya unywaji maziwa kwa kuwa, jamii inaona kutumia kinywaji hicho ni kuharibu fedha.

Watalaamu wa afya wanatakiwa kutoa elimu juu ya umuhimu wa kunywa maziwa.

Alisema umuhimu wa kunywa maziwa utausikia kipindi cha wiki ya maziwa baada ya hapo hutasikia tena, mamlaka husika zinatakiwa kutoa elimu kwa jamii.

Mfanyabiashara wa machungwa wa soko la Kariakoo, Daudi Peter, alisema kwamba, kipato ni sababu ya jamii kutokunywa maziwa.

Alieleza kuwa, maziwa yanagharama kubwa kwa mtu wa kipato cha chini ni vigumu kunywa maziwa kutokana na kipato chake pakiti ndogo inauzwa 1000 na kubwa ambayo ni nusu lita 1,500.

Maadhimisho hayo ambayo yanafanyika Mkoa wa Mbeya yanalenga kufanya tafiti kuhusu tasnia ya maziwa, kujifunza namna ya kufuga ng'ombe bora wa maziwa na kugawa maziwa katika makundi mahitaji maalum kama wagonjwa katika hospitali mbalimbali.

**Faida**

**MAZIWA NI MLO KAMILI**

Maziwa ni mlo kamili, unaweza usile ugali, maji na vyakula vinginevyo kwa sababu yana protini ya kutosha, hivyo Watanzania wanapaswa kunywa maziwa kwa ajili ya afya zao.

Scanned with CamScanner

Kazi ya kuhamisha bomba la maji inchi sita ilivyokuwa ikiendelea juzi eneo la Makongo, Dar es Salaam, kupisha ujenzi wa barabara inayoanzia Chuo Kikuu Ardhi hadi Goba kwa kiwango cha lami. (Na Mpigapicha Wetu)

# Wafugaji waombewa mikopo kwa dhamana ya mifugo

**Mbunge amesema sekta ya ufugaji ni sehemu ya uchumi wa taifa, hivyo inapaswa kuwezeshwa**

**Na Patrick Mabula, Kahama**

MBUNGE wa Jimbo la Kahama, Jumanne Kishimba (maarufu kwa jina la profesa) ameziomba taasisi za fedha zikiwemo benki kuweka utaratibu wa kuwapatia mikopo wafugaji kwa kuweka dhamana ya mifugo yao zikiwemo ng'ombe nao waweze kunufaika na fursa hiyo.

Akizungumza katika maonyesho ya biashara ya wajasiriamali na makampuni mbalimbali juzi yaliyokuwa yanafanyika katika Kituo cha Biashara na Uwezeshaji Manispaa ya Kahama alizitaka taasisi za fedha kuwakopesha mikopo wafugaji kwa kuweka dhamana ya mifugo yao.

Kishimba alisema, sekta ya wafugaji wa mifugo ni sehemu ya uchumi wa taifa, hivyo inapaswa kuwezeshwa na kuziomba taasisi za fedha katika utaratibu wao kuangalia mpango wa kuwapatia mikopo kwa kuweka dhamana ya ng'ombe badala ya nyumba.

"Kama mfugaji anatumia ng'ombe kutoa mahari na akapewa mwanamke akaoa na kukaa naye maisha yake yote sasa kwa nini benki wasimpatie mkopo kwa kuweka dhamana ya mifugo yake hiyo hiyo katika kumwendeleza kiuchumi," alisema Kishimba.

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Philimon Sengati akiongea na washiriki wa maonyesho hayo ya biashara na wananchi alisema, Serikali siku zote itaendelea kuondoa vikwazo na kuweka mazingira mazuri ya biashara kwa wawekezaji katika kuboresha kazi zao na kuchangia pato la taifa.

Sengati alisema, maonyesho hayo yaliyokuwa yamejumuisha wajasiriamali wa ndani na nje ya nchi kutoka Afirika Mashariki na Kati wanapaswa kutumia fursa hiyo ya elimu waliyopata toka kwa makampuni ya uwezeshaji kiuchumi kuwa na maono na ubunifu mpya katika kukuza shughuli zao.

"Mkoa wa Shinyanga una fursa nyingi za kiuchumi, serikali itaendelea kuwasaidia na kushirikiana na taasisi zote za umma na za watu binafsi kwa wanaotaka kuwekeza ili mkoa wetu usonge mbele katika suala la maendeleo," alisema Senga.


## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

Kadi ya pikipiki yenye usajili namba MC 119 CNB aina ya KINGLION rangi nyekundu, chasis namba L7GPCKLY1I1012467, injini namba KL162FMJ-L5012467, kwa jina la **IDDI HALFANI SIGARA** imepotea. Taarifa imetolewa kituo cha Polisi Kigoma na kupewa jalada namba KG/CPS/BVI/VOL49/2021. Kwa yeyote atakayeokota kadi hiyo anaombwa aipeleke kituo chochote cha polisi kilicho karibu.


mzuri ya Mu kuong mbali tunav Luteni Kwa Ruwa Lugor yao y bajeti wa m kwa kuchu wa m

Scanned with CamScanner

# Wawekezaji waiomba Serikali kudhibiti uvamizi ranchi za taifa

Na Mbaraka Kambona, Dodoma

WAWEKEZAJI wa muda mrefu katika Vitalu vya Ranchi za Taifa wameiomba Serikali kuchukua hatua za haraka kudhibiti uvamizi unaofanywa na baadhi ya Wananchi katika maeneo hayo kwani vitendo hivyo vimekuwa kikwazo kikubwa katika kuendeleza Sekta ya Mifugo nchini.

Wawekezaji wamesema hayo kwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki alipokutana nao katika kikao kilichoandaliwa na Kampuni za Ranchi za Taifa (NARCO) kilichofanyika jijini Dodoma Mei 29, 2021.

Wakieleza changamoto wanazozipata katika uwekezaji wao walisema kuwa pamoja na mambo mengine, suala la Wananchi kuvamia maeneo yao waliyowekeza linakwamisha kufanya shughuli zao za kuendeleza ufugaji wa kisasa.

Mwenyekiti wa Wawekezaji hao, Jackson Mwasonga alisema kuwa wavamizi wanakwamisha shughuli zao na kuna wakati wanalazimika kutoa hela kwa wavamizi hao ili waweze kuchunga mifugo yao katika maeneo wanayoyomiliki kihalali.

"Waziri inafika wakati tunatoa hela ili tuweze kuchunga na kunusuru mifugo yetu, uvamizi unatishia maisha yetu na mali zetu, tunaomba mtangaze wavamizi waondoke ili tuweze kufanya ufugaji unaohitajika kwa amani," amesema Mwasonga

Projestus Gamasho, Mwekezaji katika Ranchi ya Kitengule, mkoani Kagera alisema ranchi hiyo kwa sasa imevamiwa na tembo zaidi ya Mia Sita (600) na wameharibu miundombinu yote huku akiiomba Serikali kutoa msaada wa haraka kuwaondoa tembo hao.

Mwekezaj wa Ranchi ya Uvinza, Kigoma, Benard Katamba amesema wavamizi katika Ranchi hiyo sio tu wamechukua maeneo yao, wanaiba mifugo yao kila wakati jambo ambalo linawakatisha tamaa ya kuendelea na ufugaji.

"Sisi wawekezaji wa Ranchi ya Uvinza tumevamiwa haswa, mpaka sasa nimeshaibiwa ng'ombe 25 na mbuzi 150 na sina matumaini yoyote ya kuwapata, kwa kweli tunaomba msaada wa Serikali," amesema Katamba

Kufuatia hali hiyo, mwekezaji katika Ranchi ya Misenyi, Mkoani Kagera, Nestory Lugakingira akitoa ushauri kwa Serikali alisema kuwa ili waweze kuishi kwa amani Serikali ione uwezekano katika yale maeneo yaliyovamiwa yagawiwe kwa wavamizi hao na sehemu itakayobaki waitumie kuendeleza mifugo yao na kuepuka migogoro na wananchi hao.

Akitoa ufafanuzi wa hoja za Wawekezaji hao, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki alisema kuwa Serikali ipo pamoja na Wawekezaji hao na itachukua hatua kali kwa wale wote wanaovamia maeneo ya ranchi kinyume na Sheria.

"Ninaelewa kwamba kuna maeneo ambayo Wananchi wanakaa na kuwaondoa itakuwa ni uvunjifu wa haki za binadamu, maeneo hayo tutayainisha na ili tuone kama tunataka kuendelea nayo au tukubali maeneo hayo yawe na matumizi mengine," amesema Ndaki


Aidha,Ndaki ametumia fursa hiyo kuwahimiza Wawekezaji hao kuyatumia maeneo waliyowekeza kwa malengo yaliyokusudiwa huku akisema kuna baadhi ya Wawekezaji wamekuwa hawayatumii vizuri maeneo hayo jambo lililopelekea kuvamiwa.

"Niwaombe kuanzia sasa mkayatumie maeneo hayo kwa malengo yaliyokusudiwa,mkafanye ufugaji wa kibiashara, mkifanya hivyo mtaweza kuainisha vizuri gharama za matumizi na faida mnayopata," amesisitiza Ndaki

Naye,Mwenyekiti wa Bodi ya NARCO, Paul Kimiti alisema uvamizi unaoendelea unawaumiza Wawekezaji na kuwakatisha tamaa huku akiiomba Serikali kuchukua hatua kudhibiti vitendo hivyo.

Naiomba Serikali kuangalia uwezekano wa NARCO kuwa na Askari kama TANAPA, naamini watasaidia kudhibiti uvamizi huu kabla haujashamiri, na vitendo hivyo vitakoma," amesema Kimiti

Lengo la kikao hicho kilichoandaliwa na NARCO ni kuongea na Wawekezaji hao kuhusu Tozo mpya ya pango ya kitalu itakayoanza kufanyakazi Julai 1, 2021 na kuwahimiza kuhuisha mikataba yao.



**Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki (kulia) akiongea na Mbunge wa Jimbo la Monduli, Fredy Lowassa (kushoto) walipokutana katika kikao kilichoandaliwa na Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO) kilichofanyika jijini Dodoma juzi. Mbunge huyo alikuwa ni miongoni mwa wawekezaji waliohudhuria kikao hicho.** (Na Mpigapicha Wetu)

Scanned with CamScanner

a
uni
uu
nalinze
va
ze
ani,
ataraji
mika
ı.
nilo la
nilo ni
va awali
kwa miti,
kwa
viroba,
nza

# DC Njombe awashauri wananchi kujikita kwenye ufugaji

**Na Omary Mtamike, Njombe**

MKUU wa Wilaya ya Njombe, Ruth Msafiri amewataka wananchi wa Mkoa wa Njombe na Tanzania kwa ujumla kuingia kwenye shughuli za ufugaji kwa sababu unalipa na hautumii muda mwingi wa mfugaji.

Msafiri aliyasema jana shambani kwake baada ya kutembelewa na timu ya wataalam kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Wawakiloshi wa mradi wa utafiti wa malisho unaozingatia utunzaji wa Mazingira (CIAT) na wafugaji na wazalishaji wa malisho kutoka mikoa ya Njombe, Tanga na Kilimanjaro.

"Mfano mimi hapa kila mwezi kwa ng'ombe jike niliyenaye hapa nina uhakika shilingi 200,000 na zaidi kwa mwezi na kinyesi cha ng'ombe hawa natumia kama mbole kwenye mashamba yangu ambayo tangu nianze ufugaji sijawahi kutumia mbolea za kisasa," alisema.

Aidha Msafiri alibainisha ukosefu wa soko la uhakika la maziwa kama moja ya changamoto zinazowakabili wafugaji mkoani Njombe ambapo amesema kuwa bei ya lita moja ambayo viwanda vinanunua maziwa kwa wafugaji ipo chini ulilinganisha na bei iliyopo mtaani.

Akizungumzia kuhusu uhimilishaji Msafiri ameisifia teknolojia hiyo kwa kurahisisha upatikanaji wa ng'ombe bora na wa kisasa ambapo aliiomba Wizara kupeleka wataalam wa kutosha wa teknolojia hiyo hasa kwenye ngazi ya kata wanakopatikana wafugaji wengi.

"Bado wataalam wetu kwa upande wa hii teknolojia ni wachache na hata mimi hapa kwangu ng'ombe ameingia joto mara mbili lakini mtaalam ni mmoja na anatoka mbali hivyo kila akifika hapa anakuwa amechelewa na hapo natakiwa kusubiri tena mwezi mwingine," alisisitiza Msafiri.

Kwa upande wake kiongozi wa timu ya wataalam wa mradi wa "CIAT" An Notenbaert mbali na kufurahishwa na kazi nzuri iliyofanywa na wanifaika wa mradi huo, amewapongeza wafugaji wa Mkoa wa Njombe waliowezeshwa na mradi huo kwa kazi kubwa waliyofanya ambapo alimpa zawadi ya mbegu za malisho ya "brachiaria" aina ya kobra, mulato II na Cayman Mkuu wa Wilaya ya Njombe, Ruth Msafiri baada ya kuvutiwa na jitihada zake katika tasnia ya ufugaji kwa ujumla.

Akizungumza kuhusu umuhimu wa ziara hiyo, Kaimu Mkurugenzi wa Taasisi ya Utafiti wa Mifugo (TALIRI) Dkt. Jonas Kizima amesema kuwa ni lazima wafugaji wabadilike na kutambua kuwa ufugaji wa ng'ombe wengi bila kutenga maeneo ya kuzalisha malisho hauna tija na unasababisha migogoro baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa Ardhi.

"Wafugaji ni lazima wajue kuwa ili ng'ombe aweze kuzalisha maziwa kwa wingi anapaswa kupewa malisho bora na ndio maana unaona wakati wa kiangazi uzalishaji wa maziwa hupungua hadi asilimia 50 kwa sababu wafugaji wengi hutegemea malisho yanayostawi wakati wa masika hivyo sasa ni lazima tubadilike kwa sababu haya malisho pia imeshakuwa ni biashara nzuri sana hata kwa mtu asiyefuga," alisisitiza Dkt.Kizima

Kwa upande wa mmoja wa wafugaji waliotembelewa na timu hiyo, Juliana Mlagala alisema kuwa ziara hiyo imemuongezea tija baada ya kujifunza mambo mbalimbali ambayo alikuwa akikosea hapo awali.

"Ufugaji kwangu ndio kila kitu kwa sababu ninasomesha watoto na kufanya shughuli zote za maendeleo na leo nimejifunza zaidi kuwa sisi wafugaji hatupaswi kugeuza mifugo yetu kama dhamana ya kukopa bali tuitumie kupata fedha ambazo zitatufanya tukidhi mahitaji yetu" alihitimisha Mlagala.

Ziara hiyo itaendelea katika mikoa ya Tanga na Kilimanjaro ambapo imejikita kuweka mkazo zaidi katika suala zima la uzalishaji malisho ya mifugo.

Waziri wa

Scanned with CamScanner

ambao walijiunga na Mfuko huo baada ya kupatiwa elimu ya hifadhi ya jamii.

Taarifa hiyo njema ilitolewa mwishoni mwa wiki na Kaimu

# Wafugaji wadogo kupewa mikataba ya miaka mitatu

**Na Joyce Kasiki,Dodoma**

WIZARA ya mifugo na uvuvi imesema,ipo kwenye mpango wa kutoa mkataba wa miaka mitatu mitatu kwa wafugaji wadogo kwenye Ranch za Taifa (NARCO) ili kutatua migogoro, lakini pia kuwafanya wawe wafugaji wakubwa.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki wakati akizungumza na wawekezaji wa Ranch za Taifa pamoja na Menejimenti ya Narco.

"Kwenye Ranch za Taifa tuna matatizo mengine ya migogoro ya wafugaji na wakulima, wafugaji na watu wengine na tumesema hivi tunataka kupunguza migogoro ya wafugaji kwa kuyatoa mashamba ambayo hayatumiki kwa wafugaji wadogo wanaohamahama,"alisema Ndaki na kuongeza;

"Tulikuwa na wazo la kuwapa mkataba wa mwaka mmoja mmoja, lakini hatujui uwezo wao, lakini tumekubaliana kuwapa mikakataba ya miaka mitatu ili awe mfugaji mkubwa baadaye na lengo la kufanya hivyo tunataka akue ili tuweze kumuongeza mkataba, nia ni kutaka kutumia NARCO na mashamba yetu ili kubadilisha mashamba na aina ya ufugaji tunaofanya."

Alisema,lengo la wao kuwekeza na mfanyabiarsha yeyote ni kupata faida, hivyo wafuge kisasa ili waweze kuona faida lakini pia kuiwezesha sekta ya mifugo kuchangia vyema katika pato la Taifa.

Katika hatu nyingine Ndaki alisema, Wizara yake itailinda Ranch ya Taifa NARCO na kufanya maboresho na kuondoa vikwazo mbalimbali ili ilete tija katika sekta hiyo.

"Moja ya jambo ambalo mnatakiwa kulifanya ni kujiendesha kibiashara hamuwezi kujiendesha kibiashara ikiwa kuna vikwazo,"alisema na kuongeza;

"Kuanzia leo naomba wafugaji wa Tanzania tunakoenda wote tutafuga kila nchi,isitokee ndani ya miaka mitano, tukiendelea kufuga kiasili tutafika mahali tutalazimishwa tufuge katika eneo maalum maana mifugo na matumizi ya ardhi yanaongezeka kila siku."

